**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA KUMI NA NNE

# YATOKANAYO NA KIKAO CHA PILI

**30 JANUARI, 2019**

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**KIKAO CHA PILI – TAREHE 30 JANUARI, 2019**

## I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mwenyekiti) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

**IDADI YA WABUNGE WALIOHUDHURIA:**

**MAKATIBU MEZANI:**

1. Ndg. Lawrence Makigi
2. Ndg. Pamela Pallangyo
3. Ndg. Yona Kirumbi

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Aliweka Mezani Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 *[The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018].*

Aliweka Mezani Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 *[The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Aliweka Mezani Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 *[The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018].*

Aliweka Mezani Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 *[The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018].*

## MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Aliweka Mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 *[The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018].*

Aliweka Mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 *[The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018].*

# III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 11: Mhe. Anne Kilango Malecela

Nyongeza: Mhe. Anne Kilango Malecela
Mhe. James Francis Mbatia
Mhe. Deogratias Francis Ngalawa

Swali Na. 12: Mhe. John Wegesa Heche

Nyongeza: Mhe. John Wegesa Heche
Mhe. Catherine Valentine Magige
Mhe. Abdallah Majula Bulembo
Mhe. Ruth Hiyob Mollel

Swali Na. 13: Mhe. Almas Athuman Maige

Nyongeza: Mhe. Almas Athuman Maige

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Swali Na. 14: Mhe. Hamida Mohamed Abdallah

Nyongeza: Mhe. Hamida Mohamed Abdallah
Mhe. Mchg. Peter Simon Msigwa
Mhe. Felister Aloyce Bura

Swali Na. 15: Mhe. Vedasto Edgar Ngombale

Nyongeza: Mhe. Vedasto Edgar Ngombale
Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Swali Na. 16: Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi

Nyongeza: Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi
Mhe. Nuru Awadh Bafadhili

Swali Na. 17: Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe

Nyongeza: Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Swali na. 18: Mhe. Edwin Mgante Sannda

Nyongeza: Mhe. Edwin Mgante Sannda

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na. 19: Mhe. Mwatumu Dau Haji

Nyongeza: Mhe. Mwatumu Dau Haji
Mhe. Mendrad Lutengano Kigola
Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Mhe. Venance Methasulah Mwamoto
Mhe. Yussuf Salim Hussein

Swali Na. 20: Mhe. Anna Richard Lupembe

Nyongeza: Mhe. Anna Richard Lupembe

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Swali Na. 21: Mhe. Timotheo Paul Mnzava

Nyongeza: Mhe. Timotheo Paul Mnzava
Mhe. Flatei Gregory Massay
Mhe. Hussein Nassor Amar

Swali Na. 22: Mhe. Issa Ali Mangungu (kwa niaba yake Mhe. Abdallah Ally Mtolea)

Nyongeza: Mhe. Abdallah Ally Mtolea
Mhe. Mariam Nassoro Kisangi
Mhe. Peter Ambrose Lijualikali

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Swali Na. 23: Mhe. John John Mnyika (Kwa niaba yake Mhe. Mchg. Peter Simon Msigwa)

Nyongeza: Mhe. Mchg. Peter Simon Msigwa

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

Swali Na. 24: Mhe. Khadija Nassir Ali

Nyongeza: Mhe. Khadija Nassir Ali

**WIZARA YA NISHATI:**

Swali Na. 25: Mhe. Augustino Manyanda Masele

Nyongeza: Mhe. Augustino Manyanda Masele

## IV. MATANGAZO:

1. Wageni

   (a) Mgeni katika Jukwaa la Spika ni Mhe. Abdallah H. Makame (Mb) – Mwenyekiti wa Wabunge wa Tanzania wa Bunge la Afrika Mashariki;

   (b) Wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na Wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni walitambulishwa.

2. Matangazo ya kazi

   Matangazo mbalimbali kuhusu shughuli za kazi za Bunge yalitolewa.

## V. MWONGOZO WA SPIKA:

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitumia Kanuni ya 48 kuomba shughuli za Bunge zisitishwe kwa muda ili Bunge lijadili jambo la dharura kuhusu kubomolewa kwa Msikiti katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Mwenyekiti wa Bunge alitoa Mwongozo kwamba, suala hili limeshajadiliwa na kuwasilishwa kwa Rais na Viongozi wa dini na pia mamlaka mbalimbali za Wizara na Mkoa wa Dodoma zimeshaanza kulishughulikia. Ameomba Mhe. Jaku awe na subira wakati suala hilo likitafutiwa ufumbuzi.

## VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

1. Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania mwaka 2018 *[The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018].*

    (a) Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano - Mhe. Eng. Isack Kamwele alisoma maelezo ya Muswada;

    (b) Mhe. William Dua Nkurua kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati alisoma Maoni na Mapendekezo ya ya Kamati kuhusu Muswada;

    (c) Mhe. James Francis Mbatia kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano aliwasilisha Maoni ya Kambi hiyo kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa mwaka 2018.

2. Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 *[The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018].*

    (a) Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano - Mhe. Eng. Isack Kamwele aliwasilisha na kutoa Maelezo ya Muswada;

    (b) Mhe. Dkt. Chuachua Mohamed Rashid kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu aliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada;

    (d) Mhe. James Francis Mbatia kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano aliwasilisha Maoni ya Kambi hiyo kuhusu Muswada.

Uchangiaji wa jumla ulianza na Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchangia Miswada iliyosomwa kwa Mara ya Pili:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. James Francis Mbatia | - | NCCR |
| 2. Mhe. Magdalena Hamis Sakaya | - | CUF |
| 3. Mhe. Dkt. Diodorus Buberwa Kamala | - | CCM |
| 4. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum | - | CCM |
| 5. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko | - | CCM |

**KUSITISHA BUNGE:**

Saa 7:00 mchana, Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Mussa Azzan Zungu alisitisha Shughuli za Bunge hadi saa 10:00 jioni.

**BUNGE KUREJEA:**

Saa 10:00 jioni Bunge lilirejea likiongozwa na Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Mussa Azzan Zungu.

Mjadala kuhusu Miswada ya Sheria ya Serikali uliendelea ambapo Wabunge wafuatao walichangia:-

| | | |
|---|---|---|
| 6. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma | - | CCM |
| 7. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi | - | CHADEMA |
| 8. Mhe. Eng. Ramo Malata Makani | - | CCM |
| 9. Mhe. Moshi Selemani Kakoso | - | CCM |

**KUHITIMISHA HOJA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye | - | NW/UUM |
| 2. Mhe. Elias John Kwandikwa | - | NW/UUM |
| 3. Mhe. Prof. Adelardus Lubango Kilangi | - | AG |
| 4. Mhe. Eng. Isaack Aloyce Kamwelwe | - | W/UUM |

**KAMATI YA BUNGE ZIMA:**

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Bunge Zima kwa ajili ya kupitisha Miswada yote iliyowasilishwa Ibara kwa Ibara. Pamoja na mapendekezo ya

marekebisho yaliyowasilishwa na Mhe. Ruth Hiyob Mollel na Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi katika baadhi ya ibara, Bunge lilipitisha ibara zote zote za Muswada pamoja na marekebisho ya Serikali.

**BUNGE KUREJEA:**

Kamati ya Bunge Zima kwa Miswada yote ilikamilisha kazi yake, Bunge lilirejea na watoa Hoja walitoa Taarifa ya kazi ya Kamati ya Bunge Zima na kutoa Hoja ya kuomba Bunge likubali kupitisha Muswada.

**KUAHIRISHA BUNGE:**

Saa 12:07 jioni, Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Mussa Azzan Zungu aliahirisha Bunge hadi siku ya Alhamisi tarehe 31 Januari, 2019 saa 3:00 asubuhi.